Ufarisayo – (Phariseeism)

Na

Ellis P. Forsman

Ufarisayo – (Phariseeism)

Na

Ellis P. Forsman

Octoba 14, 2011

Ufarisayo

Mathayo 23:

Ufarisayo, hatari

Ufarisayo, uhalalishaji, na haki binafsi ni matamshi tofauti zinazotumika kuonyesha wokovu wa kupata badala ya wokovu kulingana na neema ya Mungu.

Sio Mafarisayo wote wanafanana na wale wanaonyeshwa katika Mathayo 23.

- **Nikodemo.** Yohana 3:1-2, "*Basi palikuwa na mtu mmoja wa Mafarisayo, jina lake Nikodemo mkuu wa Wayahudi. Huyo alimjia usiku akamwambia, Rabi, twajua ya kuwa u mwalimu umetoka kwa Mungu; kwa maana hakuna mtu awezaye kuzifanya ishara hizi uzifanyazo wewe isipokuwa Mungu yu pamoja naye.*"

- Yohana 19:38-40, "*Hata baada ya hayo Yusufu wa Arimathaya, naye ni mwanafunzi wa Yesu, lakini kwa siri kwa hofu ya Wayahudi, alimwomba Pilato ruhusa ili auondoe mwili wake Yesu. Na Pilato akampa ruhusa. Basi akaenda akauondoa mwili wake. Akaenda Nikodemo naye, yule aliyemwendea usiku hapo kwanza, akaleta machanganyiko ya manemane na uudi, yapata ratli mia. Basi wakautwaa mwili wake Yesu, wakaufunga sanda ya kitani pamoja nay ale manukato, kama ilivyo desturi ya Wayahudi katika kuzika.*"

Paulo alikuwa Mfarisayo, na alisimama nao katika mambo fulani dhidi ya Masadukayo.

Mdo. 23:6, "*Paulo alipotambua ya kuwa sehemu moja ni Masadukayo, na sehemu ya pili ni Mafarisayo, akapaza sauti yake katika ile baraza, ndugu zangu mimi ni Farisayo, mwana wa Farisayo; mimi ninahukumiwa kwa ajili ya ufufuo wa wafu.*"

Chachu ya Mafarisayo

Yesu alionya juu ya chachu ya Mafarisayo.

Mat. 16:6, "*Yesu akawaambia, angalieni, jilindeni na chachu ya Mafarisayo na Masadukayo.*"

Alitaja milolongo ya ole kwao. (Mat. 23).

Vipi kuhusu Ufarisayo leo?

Kuna baadhi ya watu wanaohisi kwamba kama wakimwita mtu kuwa ni Farisayo, kihualisia wanasamehewa kwa kuamini au kufanya yale mambo yanayo fundishwa na "Farisayo."

Mafarisayo walishindania mambo fulani na kupinga mambo fulani, hivyo watu wanadhani kuwa hawapaswi kusikiliza mvutano huo.

Hataivyo, wakati ukweli wa Mungu unapofundishwa lazima iangaliwe pasipokujali ni nani wanaoishindania.

Angalia kile alichokisema Yesu kuhusiana na Mafarisayo walipopinga sheria ya Musa, na sio desturi zao.

Mat. 23:1-3, "*Kisha Yesu akawaambia makutano na wanafunzi wake, akasema, akasema Waandishi na Mafarisayo wameketi katika kiti cha Musa; basi yo yote watakatowaambia, myashike na kuyatenda; lakini kwa mfano wa matendo yao, msitende; maana wao hunena lakini hawatendi.*"

Wakati Farisayo anapofundisha ukweli mtu anapaswa kusimama, kama ilivyokuwa kwa Farisayo katika mambo haya, na katika kupinga makosa katika mambo hayo.

Paulo alisimama na Mafarisayo katika mvutano kati ya Mafarisayo na Masadukayo kuhusiana na malaika, roho, na ufufuo.

Mdo. 23:6, "*Paulo alipotambua ya kuwa sehemu moja ni Masadukayo, na sehemu ya pili ni Mafarisayo, akapaza sauti yake katika ile baraza, ndugu zangu mimi ni Farisayo, mwana wa Farisayo; mimi ninahukumiwa kwa ajili ya ufufuo wa wafu.*"

Msimamo wa Kupatikana na Hatia Siyo Ufarisayo

Kuna wale wanaonekana kudhani kwamba mtu ni Farisayo mwenye fahari alipokuwa anapatikana na hatia katika imani yake ndani ya Kristo. Kwa wao hatia ni haki binafsi. Sio tu kwamba wanatweza maagizo ya Mungu, bali pia wanasema haiwezekani kuhakiki maagizo ya Mungu.

Tunaambiwa na Roho kujaribu vitu vyote, na kushikilia kile kilicho chema.

1 Thes. 5:21, "*Jaribuni mambo yote; lishikeni lililo jema.*"

Kuna wale wanaotilia shaka umakini wa kufanya kile tu ambacho Mungu ameagiza kwa kuliita Ufarisayo. Kama hili ni Ufarisayo, inakosea kufanya alichokiagiza Mungu. Kuepukana na Ufarisayo katika mtazamo

huu, mtu anapaswa kukataa mapenzi ya Mungu na kufuata matakwa yake au ya mtu mwingine.

Lakini Yesu alikemea kulifanya neno la Mungu kuwa bure ili kwamba mtu aweze kushika maagizo ya wanadamu.

Mat. 15:8-9, "*Watu hawa hunieshimu kwa midomo, ila mioyo yao iko mbali nami. Nao waniabudu bure wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu.*"

Hivyo basi, kuna kitu hakipo sawa na hii tafsiri ya Ufarisayo.

Watu wengine wananyooshea kidole ole katika Mathayo 23:23:

Mat. 23:23, "*Ole wenu waandishi na Mafarisayo wanafiki! Kwa kuwa mnalipa zaka za manana na bizari na jira, lakini mmeacha mambo makuu ya sheria, yaani adili na rehema, na imani; hayo imewapasa kuyafanya, wala yale mengine msiyaache.*"

Hakuhukumu umakini wao katika fungu la kumi. Walipaswa kufanya hivyo, alisema. Hataivyo, hakuwahukumu kwa kuacha kufanya mambo makubwa ya sheria bila kuyafanya. Walipaswa kufanya yote.

Zaidi sana, waliongeza katika mapenzi ya Mungu maagizo ya wanadamu. Walishikilia maagizo haya juu ya mapenzi ya Mungu.

Marko 7:1-12, "*Kisha Mafarisayo, na baadhi ya waandishi waliotoka Yerusalemu, wakakusanyika mbele yake, wakaona wengine katika wanafunzi wake wakila vyakula kwa mikono najisi, yaani isiyonawiwa. Kwa maana Mafarisayo na Wayahudi wote wasiponawa mikono mpaka kiwiko, hawali wakishika mapokeo ya wazee wao; tena wakitoka sokoni wasipotawadha, hawali, na yako mambo mengine waliyopokea kuyashika, kama kuosha vikombe na midumu, na vyombo vya shaba. Basi wale Mafarisayo na waandishi wakamwuliza mbona wanafunzi wako hawaendi kwa kuyafuata mapokeo ya wazee, bali hula chakula kwa mikono najisi? Akawaambia Isaya alitabiri vyema juu yenu ninyi wanafiki, kama ilivyoandikwa, watu hawa hunieshimu kwa midomo, ila mioyo yao iko mbali nami; nao waniabudu bure wakifundisha mafundisho yaliyo mapokeo ya wanadamu, ninyi mwaiacha amri ya Mungu na kuyashika mapokeo ya wanadamu. Akawaambia vema! Mwaikataa amri ya Mungu mpate kuyashika mapokeo yenu. Maana Musa alisema waheshimu baba yako na mama yako, na amtukanaye babaye au mamaye kufa na afe. Bali ninyi husema mtu akimwambia babaye au mamaye, ni Korbani yaani wakfu, kitu change chochote kikupasacho kufaidiwa nacho huwa basi; wala hammruhusu baada ya hayo kumtendea neno babaye au mamaye:*"

Wayahudi walikuwa na mambo mengi yaliyoandikwa na wazee wao walioyafuata hata kwa karibu kuliko maneno yaliyoandikwa na Musa. Yesu aliongea juu ya mapokeo haya. ilikuwa ni hii "sheria" Mafarisayo walikuwa wanaongelea Mathayo anamaliza tofauti ndogo hii.

Mat. 15:11, 20, "*Sikilizeni mfahamu, sicho kiingiacho kinywani kimtiacho mtu unajisi; bali kitokacho kinywani ndicho kimtiacho mtu unajisi. Hayo ndiyo yamtiayo mtu unajisi; lakini kula kabla hajanawa hakumtii mtu unajisi.*"

Alikuwa anaongelea Mafarisayo walikuwa wanalalamikia kuhusu uchafu wa mikono yao na vyombo walivyo kuwa wanatumia. Hii haikuhusiana na chochote kilichokwenda ndani ya mtu. Vitu vingine vinavyoutia mtu unajisi vilifunikwa katika Biblia sehemu fulani. Mungu amefunika kwa maksudi mara nyingi katika Agano Jipya na Agano la Kale matokeo ya kunywa pombe iliyo changanywa. 1 Kor. 6:10 inatuambia kwamba walevi hawataurithi ufalme wa Mungu. Kimsingi hiyo inavitu ninavyochafua.

Mafarisayo waliongeza mapokeo ya wazee katika Sheria ya Musa. Ni mapokeo haya ndiyo Kristo alikuwa anapinga. Tunapaswa kutunza mapenzi ya Mungu.

Mtu lazima awe mwangalifu asije akajaribu kuthibitisha kwamba siyo Farisayo kwa kujiweka huru na sheria yote au mifumo ya Mungu. Mtu akifanya hili anajaribu kujithibitisha mwenyewe; maana haegemei katika kile ambacho Mungu amekisema, bali katika mawazo yake mwenyewe.

Chini Ya Hakuna Sheria?

Je ni Ufarisayo kushikilia kwa Mkristo yuko chini ya sheria kwa mtazamo fulani? Kama sheria haitendi kazi kwa Mkristo, tunakabiliwa na hitimisho zifuatazo:

Hakuna chochote ambacho Mkristo anaweza kufanya na hakuna chochote ambacho Mkristo anaweza kuacha kufanya.

Lakini 1 Yohana 3:4 inasema, "*Kila atendaye dhambi afanya uasi; kwa kuwa dhambi ni uasi.*"

Kama hakuna sheria, hakuna uvunjifu wa sheria, na hivyo hakuna dhambi. Mkristo kwa mtazamo huu anaweza kutoa ushahidi wa uongo, kuiba, au kuzini kwa sababu hakuna sheria.

Kama wana sheria, ni sheria dhidi ya kile wanachodhani Ufarisayo ndiyo, ambayo ndiyo mkanganyiko, kwa sababu tena wanasheria.

Neema, Siyo Sheria

Wengine wananukuu Rum. 6:14, "*Kwa maana dhambi haitawatawala ninyi, kwa sababu hamwi chini ya sheria, bali chini ya neema.*"

Hii ilikuwa ni sheria ya Musa. Wayahudi wa kindi kile walielewa kile ambacho Paulo alikuwa akisema.

Je Paulo anamanisha kwamba sheria haimhusu Mkristo? Anaongelea dhambi kututawala. Kama yote tuliyonayo ilikuwa sheria, wote tungekuwa kwenye dhambi kwa sababu wote tunatenda dhambi, na sheria haiwezi kuondoa dhambi. Dhambi inaweza kuwa ndani yetu na kututawala hadi kufa. Ni neema ya Mungu ndiyo huondoa uwepo wa dhambi ndani yetu. Neema hutolewa na Mungu; lakini hii haituondowi katika kuishi chini ya sheria yake ya Neema. Pia alitupatia neema yake. Kama tukiikata neema yake leo, basi tunaigeuza neema kuwa leseni ya kutenda dhambi.

Hakusema <u>wanaweza</u> wasitende dhambi, alisema <u>hawapaswi</u> kutenda dhambi.

- Rum. 6:16-18, "*Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake, kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti, au kwamba ni utumishi wa utii uletao haki. Lakini Mungu na ashukuriwe kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mliitii kwa mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake; na mlipokwisha kuwekwa huru mbali na dhambi, mkawa watumwa wa haki.*"
- Rum. 6:23, "*…mshahara wa dhambi ni mauti;…*"

Sheria Ipo Katika Mafundisho Ya kKweli

Biblia iko wazi kwamba sheria inamhusu Mkristo. Tunapaswa kutenda mapenzi ya Mungu ili kuweza kuingia katika ufalme wa Mungu.

Mat. 7:21-23, "*Si kila mtu aniambiaye Bwana, Bwana, atakayeingia katika ufalme wa Mbinguni; bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliyembinguni. Wengi wataniambia siku ile, Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, sikuwajua ninyi kamwe, ondokeni kwangu ninyi mtendao maovu.*"

Kuna wengine wanaohisi kwamba wapo kiroho katika kujitweza wazo la amri kufungwa kwa Wakristo.

Paulo aliandika katika 1 Kor. 14:37, "*Mtu akijiona kuwa ni nabii au mtu wa rohoni, na ayatambue hayo ninayowaandikia, ya kwamba ni maagizo ya Bwana.*"

Kuna maagizo ya Mungu. **Tunatakiwa** kuziangalia.

Mat. 28:20. "*Na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari.*"

Siyo alama ya kiroho kuwa tofauti na wao.

Kumpenda Mungu haipaswi kutohusishwa na amri zake. Yohana 14:15, "*Mkinipenda mtazishika amri zangu.*"

Ambavyo Ufarisayo Hakika Ulivyo

Unafiki. Luka 12:1, "*Wakati huo makutano walipokutanika elfu elfu, hata wakakanyagana, alianza kuwaambia wanafunzi wake kwanza, jilindeni na chachu ya Mafarisayo ambayo ni unafiki.*"

Kutazamwa na watu. Mat. 23:1-7, "*Kisha Yesu akawaambia makutano, na wanafunzi wake akasema, Waandishi na Mafarisayo wameketi katika kiti cha Musa; basi yo yote watakatoyowaambia, myashike na kuyatenda; lakini kwa mfano wa matendo yao, msitende, maana wao hunena lakini hawatendi. Wao hufunga mizigo mizito na kuwatwika watu mabegani mwao; wasitake wenyewe kuigusa kwa kidole chao. Tena matendo yao yote huyatenda ili kutazamwa na watu kwa kuwa hupanua hirizi zao, huongeza matamvua yao; hupenda viti vya mbele katika karamu, na kuketi mbele katika masinagogi, na kusalimiwa masokoni, na kuitwa na watu Rabi.*"

Hali ya moyo wa Farisayo ulikuwa tofauti sana na muonekano wake wa nje.

Yesu alisema walikuwa wanafunga vitu juu yaw engine ambavyo wao wenyewe walikuwa hawazifuati; na mengi ya mambo wanayofunga havikutoka kwa Mungu.

Sehemu ya matatizo yao ilikuwa ni haki binafsi, badala ya haki ya Mungu.

Kuna tofauti.

Rum. 10:1-3, "*Ndugu zangu nitakayo sana moyoni mwangu na dua yangu nimwombayo Mungu, ni kwa ajili yao ili waokolewe. Kwa maana nawashuhudia kwamba wana juhudi kwa ajili ya Mungu, lakini si katika maarifa. Kwa maana wakiwa hawaijui haki ya Mungu, na wakitaka kuthibitisha haki yao wenyewe, hawakujitia chini ya haki ya Mungu.*"

Mungu anapomwonyesha mwanadamu kazi ya kufanya, ni kwa ajili ya haki yake, siyo mwanadamu. Mwanadamu lazima azifanye, siyo kazi

zake bali ni za Mungu. Mwanadamu anaokolewa kwa kutembea katika njia ya Mungu iliyoonyeshwa. Anaokolewa kwa kufanya kazi ya Mungu, ambayo ndiyo haki yake, kwa sababu anathibitisha haki yake kwa kufanya mambo yaliyoagizwa na Mungu.

Kama. Ubatizo siyo haki ya mwanadamu, bali Mungu.

Yakobo 2:21-22, "*Je! Baba yetu Ibrahimu hakuhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo, pale alipomtoa Isaka mwanawe juu ya madhabahu? Waona kwamba imani ilitenda kazi pamoja na matendo yake, nay a kwamba imani ile ilikamilishwa kwa njia ya matendo yale.*"

Sura ya 2 ya Yakobo yote inatufundisha kwamba imani na matendo uenda pamoja; kwa sababu tunaongea kuhusu matendo na haki ya Mungu, na siyo ya mwanadamu.

- Mat. 23:23, "*Ole wenu waandishi na Mafarisayo, wanafiki! Kwa kuwa mnalipa zaka za mnanaa na bizari na jira, lakini mmeacha mambo makuu ya sheria, yaani, adili, na rehema, na imani; hayo imewapasa kuyafanya, wala yale mengine msiyaache.*"
- Rum. 10:17, "*Basi imani chanzo chake ni kusikia; na kusikia huja kwa neno la Kristo.*"

Hitimisho

Mat. 23:1-3, "*Kisha Yesu akawaambia makutano na wanafunzi wake, akasema, Waandishi na Mafarisayo wameketi katika kiti cha Musa; bali yo yote watakayowaambia myashike na kuyatenda; lakini kwa mfano wa matendo yao, msitende; maana wao hunena lakini hawatendi.*"

Mat.16:6, "*Yesu akawaambia, angalieni, jilindeni na chachu ya Mafarisayo na Masadukayo.*"